# Mbinu ya Swala ya Eid

## (Shafi'i)

(Swahili)



Presented by

Majlis Al-Madina-tul-'Ilmiyyah

Translated by

Translation Department (Dawat-e-Islami)

نمازِ عید کا طریقہ (شافعی)

Namaz-e-‘Eid Ka Tariqah (Shafi’i)

# Mbinu ya Swala ya Eid (Shaafi’i)

**KITABU** HIKI KILITOLEWA KWA KIURDU NA *Madinah al-‘Ilmiyyah.* **Idara ya Tafsiri (Dawat-e-Islami)** imekitafsiri kwa Kiswahili. Ukipata kosa lolote katika kutafsiri au kutunga, tafadhali ijulishe Idara ya Tafsiri kwenye anwani ifuatayo ya posta au barua pepe kwa nia ya kupata zawadi (*thawab*).

**Idara ya Tafsiri (Dawat-e-Islami)**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Karachi, Pakistan

**UAN:** ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ugani. 7213

**Barua Pepe:** 🖃 translation@dawateislami.net

Mbinu ya Swalah ya Eid (Shaafi'i)

Tafsiri ya Kiswahili ya 'Namaz-e-'Eid Ka Tariqah (Shafi'i)'

◆


**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA**

Hakimiliki © 2024 Maktaba-tul-Madinah

---

Hairuhusiwi kunakili, au kusambaza sehemu ya chapisho hili kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodiwa au vinginevyo, bila kibali cha maandishi cha Maktaba-tul-Madinah.


---


| | |
|---|---|
| **Uchapishaji wa kwanza:** | Muharram-ul-Haram, 1446 AH - (Aug 2024) |
| **Mchapishaji:** | Maktaba-tul-Madinah |
| **Idadi:** | --- |


## UDHAMINI

Tafadhali jisikie huru kuwasiliana nasi ikiwa ungependa kufadhili uchapishaji wa kitabu cha kidini au kijitabu kwa ajili ya Isal-e-Sawab ya wanafamilia wako waliofariki.


**Maktaba-tul-Madinah**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Karachi, Pakistan

✍**BaruaPepe:**global@maktabatulmadinah.com|feedback@maktabatulmadinah.com
✆ **Nambari ya Simu:** +92-21-34921389-93
💻 **Tovuti:** www.dawateislami.net | www.maktabatulmadinah.com

ٱلۡحَمۡدُ لِلّٰهِ رَبِّ الۡعٰلَمِیۡنَ، وَ الصَّلٰوةُ وَ السَّلَامُ عَلٰی خَاتَمِ النَّبِیّٖن،
اَمَّا بَعۡدُ فَاَعُوۡذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّیۡطٰنِ الرَّجِیۡمِ ؕ بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ ؕ

# Du'a kwa ajili ya kusoma kitabu

Soma dua ifuatayo (ombi) kabla ya kusoma kitabu cha dini au somo la Kiislamu, utakumbuka chochote unachosoma, اِنۡ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

## *Tafsiri*

**Ewe Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ! Tufungulie milango ya elimu na hekima na utuhurumie! Ewe Ambaye ni Mtukufu na mwenye Hekima**

*(Al-Mustatraf, juz. 1, uk. 40)*

**Kumbuka:** Mswalie mtume ﷺ mara moja kabla na baada ya Du'a.

# Soma hii kwanza

اَلْحَمْدُ لِلّٰه vitabu na vijitabu vilivyoandikwa na Shaykh-e-Tareeqat Ameer-e-Ahl-e-Sunnat, mwanzilishi wa Dawat-e-Islami ʻAllamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَة vinajumuisha hazina isiyokadirika ya elimu na mafundisho ya hekima juu ya imani, matendo, fadhila, ubora, Shari'ah, Tareeqah, historia, wasifu, sayansi, ushauri wa kimatibabu, adabu, tabia njema, mambo ya kawaida ya kila siku na masomo mengine mengi. Kwa hiyo, Kutub-e-Fiqh-e-Shaafi'i, idara ya Al-Madina-tul-Ilmiyyah (Kituo cha Utafiti cha Kiislamu) sasa inakusanya vitabu vyake kwa kufanya mabadiliko ya lazima kwa kuzingatia hukumu za kifiqhi ya Shaafi'i ili watu wanaofuata sheria za Shaafi'i pia waweze kupata manufaa kutokana na maandishi ya Ameer-e-Ahl-e-Sunnat, yaliyojaa elimu na hekima.

- Undani wa kazi iliyofanywa kwenye kijitabu hiki na idara ya Kutub-e-Fiqh-e-Shaafi'i ni kama ifuatavyo: Hukumu zote za kifiqhi zilizotajwa katika kijitabu hiki zimebadilishwa na zile zinazotoka katika vitabu sahihi vya shule ya mawazo ya Shaafi'i.

- Katika baadhi ya maeneo, maamuzi yameongezwa pale inapobidi.

- Mabadiliko yamefanywa kwa kuzingatia istilahi za Dawat-e-Islami na kanuni zilizosasishwa za Kituo cha Utafiti cha Kiislamu na idara, Kutub-e-Fiqh-e-Shaafi'i.

- Kijitabu kizima kimechunguzwa na Mufti Muhammad Rafeeq Sa'di Shaafi'i مَدَّ ظِلُّهُ العالی.

Sifa zote njema katika kijitabu hiki bila shaka zinatokana na uwezeshaji uliotolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, msaada wa Mtukufu Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, neema za watu watakatifu na mapenzi na dua za dhati za Ameer-e-Ahl-e-Sunnat. Kasoro yoyote itakayopatikana itatokana na uzembe wetu bila kukusudia.

Kutub-e-Fiqh-e-Shaafi'i
Idara ya Al-Madina-tul-Ilmiyyah
(Kituo cha Utafiti cha Kiislamu)
19 Jumadal Ukhra 1442 A.H. / Februari 2, 2021

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ، وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى خَاتَمِ النَّبِيّٖنَ،
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# Mbinu ya Swala ya Eid
## (Shaafi'i)

Haijalishi ni kiasi gani Shetani anajaribu kukuzuia kusoma kijitabu hiki cha kurasa 9, tafadhali kisome chote. اِنْ شَآءَاللّٰه utaona faida mwenyewe.

## Ubora wa Swala-'Alan-Nabi ﷺ

Nabii Mkuu na wa Mwisho صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kunisomea mimi Swala mara mia katika usiku wa Jumu'ah na mchana wa Jumu'ah, Mwenyezi Mungu atamtimizia haja zake mia moja; sabini za Akhera na thelathini za dunia.'[1]

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Moyo utabaki hai

Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kufanya Qiyam (yaani ibada) katika mikesha ya Idi (yaani Eid-ul-Fitr na Eid-ul-Adha) akitafuta malipo, moyo wake hautakufa siku

---

[1] *Tareekh Ibn Asakir, juz. 54, uk. 301, Hadithi 6783*

ambayo nyoyo za watu zitakufa.'[1]

## Kuingia Peponi kunakuwa Wajib

Sayyiduna Mu'aaz Bin Jabal رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ amesimulia: Mwenye kukesha (yaani akiabudu) katika mikesha mitano ifuatayo, basi amehakikishiwa Pepo: usiku wa tarehe 8, 9 na 10 Dhul-Hijjah, usiku wa Eid-ul-Fitr na usiku wa 15 Shaaban/Laylatu-Niswfi min Shaabaan. (Shab-e-Bara'at).[2]

## Sunnah kabla ya kwenda kwenye Swalah ya Eid

Sayyiduna Buraydah رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ amesimulia, 'Siku ya Eid-ul-Fitr, Mtukufu Mtume صَلَّی اللّٰہ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم angeenda kuswali swala ya Eid baada ya kula kitu; ambapo siku ya Eid-ul-Adha, hakula chochote mpaka baada ya swala ya Eid.'[3] Vile vile katika Bukhari kuna hadithi nyingine iliyopokelewa na Sayyiduna Anas رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ, 'Katika siku ya Eid-ul-Fitr, Mtukufu Mtume صَلَّی اللّٰہ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم asingeenda kuswali swala ya Eid mpaka ale tende chache kwa idadi ya witri.'[4]

## Sunnah ya kuelekea kuswali Swalah ya Eid na kurudi baada yake

Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِیَ اللّٰہ عَنۡہُ amesimulia, 'Mtukufu

---

[1] *Ibn Majah, uk. 284, Hadithi 1782, Dar-ul-Kutub al-Ilmiyyah*

[2] *Attargheeb, wa al-Tarheeb, uk. 373, Hadithi 2, Dar-ul-Ma'rifah Beirut*

[3] *Tirmizi, uk. 160, Hadithi 542 Dar-ul-Kutub Ilmiyyah Beirut*

[4] *Bukhari Kitab Al-'Aiden, uk. 289, Hadithi 953 Dar-ul-Ma'rifah Beirut*

Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم angeenda kuswali swala ya Eid kutumia njia moja na angerudi kutumia njia nyingine.'[1]

## Mbinu ya kuswali swala ya Eid (Shaafi'i)

Kwanza, fanya nia ifuatayo: Nakusudia kuswali Sunnah ya Rak'aat mbili za Eid-ul-Fitr (au Eid-ul-Adha), kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, huku uso wangu ukielekea Qiblah. Wakati wa kuswali kwa jamaa, Imam anatakiwa kukusudia Uimamu na Muqtadi awe na nia ya kumfuata (Imaam).[2] Nia ikiwa moyoni, inua mikono hadi mabegani huku ukitamka اَللهُ اَكْبَر. Na kisha kunja mikono chini ya kifua kama kawaida na usome dua ya kuanzisha swala.

Kisha, inua mikono yako hadi kwenye mabega yako huku ukitamka اَللهُ اَكْبَر, kisha ikunje chini ya kifua na usome yafuatayo:

سُبْحٰنَ اللهِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَلَآ اِلٰهَ اِلَّا اللهُ وَاللهُ اَكْبَر

Sema Takbira mara saba kwa njia ile ile. Baada ya Takbira sita za mwanzo, kunja mikono yako chini ya kifua na usome hivyo hivyo:

سُبْحٰنَ اللهِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَلَآ اِلٰهَ اِلَّا اللهُ وَاللهُ اَكْبَر

[1] *Tirmizi, uk. 159, Hadithi 541*

[2] *I'anat al-Talibeen, juz. 1, uk. 445, Dar-ul-Kutub Ilmiyyah Beirut; Al-Munhij Al-Qaweem, uk. 172, Dar-ul-Minhaj Jeddah*



www.dawateislami.net

Baada ya Takbira ya saba, Imamu na Munfarid (mwenye kuswali binafsi) watasoma Ta'awwuz kwa sauti ya chini kisha watasoma Surah al-Fatihah na Sura nyingine kwa sauti inayosikika. Na (baada ya Surah al-Fatihah, wakati Imamu anapopumzika, katika mapumziko hayo) Muqtadi atasoma Ta'awwuz na Sura al-Fatihah kwa sauti ndogo tu (asisome Sura nyingine baada yake).

Katika Rak'ah ya pili kabla ya Ta'awwuz, huku akitamka (اَللّٰهُ اَكْبَرْ) inua mikono yako hadi mabegani mwako mara tano; na, katika nne za mwanzo kabisa, kunja mikono yako chini ya kifua baada ya kila Takbira na soma

سُبْحٰنَ اللهِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَلَآ اِلٰهَ اِلَّا اللهُ وَاللهُ اَكْبَرَ. Baada ya Takbira ya tano, Imamu na Munfarid (mtendaji binafsi) watasoma Ta'awwuz kwa sauti ya chini na kisha watasoma Surah al-Fatihah na Sura nyingine kwa sauti inayosikika. Na (baada ya Surah al-Fatiha, Imam anapopumzika, katika mapumziko hayo) Muqtadi atasoma Ta'awwuz na Surah al-Fatihah kwa sauti ndogo tu kisha atakamilisha Swalah kwa mujibu wa sheria.[1] Imamu na Munfarid (mtendaji binafsi) wanaweza kusoma Sura yoyote baada ya Surah al-Fatihah; hata hivyo, ni Sunnah kusoma Surah Qaaf au Surah A'la katika Rak'ah ya kwanza na katika

[1] *Tuhfa al-Muhtaj, ma' Haashiyah Sharwani, juz. 3, uk. 494, 497; Nihayah al-Muhtaj, Kitab Salat al Jama'at, juz. 2, uk. 172 imechaguliwa Dar-ul-Kutub Ilmiyyah Beirut*



www.dawateislami.net

Rak’ah ya pili kusoma ama Surah Qamar au Surah Ghaashiyah ni Sunnah.[1]

## Hukumu ya Swalah ya Eid

Swalah za Eid zote mbili (yaani Eid-ul-Fitr na Eid-ul-Adha) ni Sunnah Mu’akkadah kwa kila Mukallaf yaani mtu mwenye kukalifishwa na Shariah (iwe mwanamume au mwanamke); na kuiacha ni Makruh.[2] Zaidi ya hayo, Azan wala Iqamat hailetwi kwa ajili ya Swala za Idi zote mbili.[3] Swala ya Eid inaweza kutolewa kwa jamaa na vile vile kibinafsi. Hata hivyo, kuiswali kwa mkusanyiko kuna ubora zaidi kwa asiyekuwa Haji. Na kwa Haji ni Mustahab kuswali mtu mmoja mmoja.[4]

**Kumbuka:** Neno Haji linamrejelea yule anayehiji sasa, sio yule aliyefanya hijja hapo awali.

## Khutba ya Eid ni Sunnah

Khutba mbili baada ya Swalah ya Eid ni Sunnah, kama ile ya Ijumaa. Hata hivyo, khutba si Sunnah kwa Munfarid (mtendaji binafsi) ambaye aliswali Eid Salah kibinafsi.[5]

---

[1] *Tuhfa al-Muhtaj, ma’ Haashiyah Sharwani, juz. 3, uk. 501*

[2] *Tuhfa al-Muhtaj, m’a Haashiyah Sha’rani, juz. 3, uk. 491*

[3] *Al-Majou’ Sharah al-Mazhab, juz. 6, uk. 67, Dar-ul-Hadith Qahirah*

[4] *Nihayah al-Muhtaj, juz. 2, uk. 173; Tuhfa Al Muhtaj, juz. 1, uk. 458*

[5] *Tuhfa al-Muhtaj, juz. 1, uk. 460*



www.dawateislami.net

## Hukmu ya Swalah ya Eid kwa wanawake

Salah za Eid (hiyo ya Eid-ul-Fitr na Eid-ul-Adha) ni Sunnah Mu'akkadah kwa wanawake pia; hata hivyo, watatoa hizi katika nyumba zao. Wanawake wanaweza kuswali Swalah ya Eid kwa pamoja majumbani mwao lakini mawaidha baada ya Swalah ya Eid sio Sunnah kwa Swalah ya jamaa ya wanawake.[1]

## Wakati wa Swala ya Eid

Wakati wa Swalah kwa Eid zote mbili huanza kutoka mawio ya jua na kuendelea hadi Zawal (jua linapoanza kushuka). Hata hivyo, wakati wa Sunnah ni pale jua linapochomoza hadi urefu wa mkuki mmoja (dakika 20 baada ya kuchomoza kwa jua). Ni Sunnah kuharakisha kuswali Swala ya Eid-ul-Adha ili iruhusu muda zaidi wa dhabihu. Ni Sunnah kucheleweshа swala ya Eid-ul-Fitr kidogo ili mtu apate muda zaidi wa kulipa Sadaqa-e-Fitr kabla ya Swalah kwa sababu wakati wa kubeba fadhila zaidi kulipa Sadaqa-e-Fitr ni wakati kati ya Fajr Salah na swala ya Eid siku ya Eid. Kwa hivyo, kuchelewesha swala ya Eid kidogo kutaruhusu wakati uliobarikiwa zaidi wa kulipa Sadaqa-e-Fitr.[2]

## Nini cha kufanya ikiwa mtu ataswali swala ya Eid kwa sehemu/ sio kwa ukamilifu?

Inapendekezwa kwa Muqtadi (mfuasi) kutenda kulingana na

---

[1] *Haashiyah Sharwani, juz. 3, uk. 492,493*

[2] *Tufa al-Muhtaj, m'a Haashiyah Sha'rani, juz. 3, uk. 493, 509*

Imam katika Takbeerat. Iwapo Imam amesema Takbiyrat tatu, basi atamke Takbira tatu pia. Iwapo Imamu ametamka Takbiyrat sita, atamke Takbira sita pia. Ikiwa Imam hakutamka Takbira, hatakiwi kutamka Takbira yoyote pia.[1]

- Masbooq i.e. Yule ambaye hakupata Takbira zote pamoja na Imam, atamke Takbirat zile tu alizoweza kumfuata Imamu. Kwa mfano, alianza Iqtida (kufuata) katika Rak'ah ya kwanza wakati ambapo ilikuwa imebaki Takbira moja tu kati ya saba, sasa atamke Takbira moja tu. Na ikiwa hakupata Takbira yoyote, hatakiwi kutamka Takbira yoyote pia.
- Vile vile, kama angemkuta Imamu kwenye Takbira ya kwanza ya Rakaa ya pili, sasa si Takbira saba bali tano, kwa mujibu wa Imamu, zitamkwe naye. Na atakaposimama Rak'ah yake ya pili, atasema Takbira tano katika hili pia kwa sababu ni Sunna kutamka Takbira mara tano katika rakaa ya pili na hii ni Rak'ah yake ya pili.[2]

## Vipi kama atatoa Swala ya Eid nyuma ya Imamu wa Hanafi?

Kwa mujibu wa Ahnaaf, Takbira tatu hutamkwa kabla ya Surah Fatihah katika Rak'ah ya kwanza na Takbiyrat tatu

[1] *Al-Munhij, Al-Qaweem, uk. 324*

[2] *Tuhfa al-Muhtaj, m'a Haashiyah Sha'rani, juz. 3, uk. 499; Al Munhij Al-Qaweem m'a Haashiyah Tarmasi, juz. 4, uk. 479, Dar-ul-Minhaj Jeddah*



www.dawateislami.net

hutamkwa kabla ya Rukuu katika rakaa ya pili. Kwa hiyo, Shaafi'i anaposwali Eid nyuma ya Imamu wa Hanafi, kwa mujibu wa kitendo cha Imamu, atatamka Takbira tatu tu katika Rakaa ya kwanza; ilhali katika Rakaa ya pili hatatamka Takbira kwa sababu sio wakati wa kutamka Takbira baada ya Surah Fatihah.[1]

## Hukumu za khutba ya Eid

Baada ya swala ya Eid, Imam atatoa khutba mbili. Matendo ambayo ni Rukn kwa khutba ya Jumu'ah pia ni Rukn ya khutba ya Eid. Matendo ambayo ni Sunnah kwa khutba ya Jumu'ah pia ni Sunnah kwa khutba ya Eid. Khutba ya kwanza itaanza kwa Takbiyrat tisa na ya pili itaanza kwa Takbiyrat saba. Asome Takbeerat kwa wingi baina ya khutba mbili hizo na ni Sunna kufundisha hukumu za Sadaqa-e-Fitr katika khutba ya Eid-ul-Fitr na hukumu za kutoa dhabihu katika khutba ya Eid-ul-Adha.[2]

## Adabu 11 za Eid

Yafuatayo ni matendo ya Sunnah katika siku ya Idi:

- kutumia mikesha ya Eid kuswali, kusoma Quran, kutaja majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuomba, na

[1] *I'anat al-Talibeen, juz. 1, uk. 445*

[2] *I'anat al-Talib'een, juz. 1, uk. 448*



www.dawateislami.net

kadhalika.; kwa kutumia sehemu kubwa ya usiku katika ibada, Sunnah hii itakamilika.

- Kuoga. Wakati wa kufanya hivi huanza kutoka usiku wa manane lakini ni bora kufanya hivi baada ya Alfajiri.[1]
- Kukata kucha; kwa kuongeza, nyoa kwapa na nywele za sehemu ya siri. (Hii si Sunnah kwa yule ambaye amekusudia kutoa dhabihu.)[2]
- Kupaka manukato mwilini na katika mavazi.
- Kuvaa nguo bora zaidi. Nguo nyeupe ni bora zaidi, lakini ikiwa nguo nzuri zaidi inapatikana, ni bora (kuvaa).[3]
- Kuswali Swala ya Eid Msikitini.
- Watu wafike mapema mahala pa Swalah ya Eid baada ya Swalah ya Fajr ili wapate ukaribu na Imamu na fadhila za kungojea Swalah.
- Kula au kunywa kitu kabla ya Swala ya Eid-ul-Fitr; ni Sunnah kula tende kwa idadi ya witri (k.m. tatu, tano, saba au zaidi).
- Kutokula chochote kabla ya Swalah ya Eid-ul-Adha (Eid ya dhabihu).

---

[1] *Al-Munhij Al-Qaweem, uk. 321,322*

[2] *Tufa al-Muhtaj, juz. 1, uk. 461*

[3] *Tufa al-Muhtaj, juz. 1, uk. 461; Haashiyah Tarmisi Ali Minhaj Al-Qayyoom, juz. 4, uk. 458*



www.dawateislami.net

- Kufanya kinyume katika hali zote mbili (yaani kutokula chochote kabla ya Swalah ya Eid-ul-Fitr na kula kitu kabla ya Swalah ya Eid-ul-Adha) ni Makruh.
- Kutembea kwa njia ya kifahari na tulivu hadi mahali palipotengwa kwa ajili ya Eid Salah. Hakuna suala kwa yule ambaye hawezi kutembea, kuchukua gari.
- Kwenda kwa njia moja kwa ajili ya swala ya Eid na kurudi kwa njia nyingine; na kuchukua njia ndefu wakati wa kwenda.[1]

## Lulu za Madani 8 kuhusu Takbira kuhusiana na herufi nane za kishazi اَللّٰهُ اَكْبَر

Ni Sunnah kwa asiyekuwa Haji kutamka Takbira kwa sauti katika mikesha ya Eid-ul-Fitr na Eid-ul-Adha, kuanzia machweo ya jua hadi pale anaposema Takbira-e-Tahrimah kwa ajili ya Swalah ya Idi. Kumbuka kwamba, mwanamke hatakiwi kutamka Takbira kwa sauti iwapo kuna mtu asiyekuwa Mahram.[2]

Maneno ya Takbira ni haya yafuatayo:

اَللّٰهُ اَكْبَرُ اَللّٰهُ اَكْبَرُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَاللّٰهُ اَكْبَرُ اَللّٰهُ اَكْبَرُ وَلِلّٰهِ الْحَمْدُ

---

[1] *Tufa al-Muhtaj, juz. 1, uk. 461,462, imechaguliwa*

[2] *I'anat al-Talib'een, juz. 1, uk. 446*



www.dawateislami.net

Ni Mustahab na imependekezwa kuongeza:

’’ اَللّٰهُ اَكْبَرُ كَبِيْرًا وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ كَثِيْرًا وَسُبْحٰنَ اللّٰهِ بُكْرَةً وَّاَصِيْلًا لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَلَا نَعْبُدُ اِلَّآ اِيَّاهُ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ وَلَوْ كَرِهَ الْكٰفِرُوْنَ لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ صَدَقَ وَعْدَهٗ وَنَصَرَ عَبْدَهٗ وَهَزَمَ الْاَحْزَابَ وَحْدَهٗ لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَاللّٰهُ اَكْبَرُ۔[1]

- Takbira ya Eid itasemwa na yule anayeswali Swalah ya Eid kwa pamoja, hadi pale Imamu atakaposema Takbiir-e-Tahrimah na kwa yule anayeitoa peke yake hadi wakati anaposema Takbiir-e-Tahrimah. Na asiyeswali Swalah ya Eid aendelee kutamka Takbira ya Eid wakati wa Zawaal (jua linapoanza kuteremka).
- Ni Sunna kutamka Takbira ikiwa mtu anatembea kwa miguu, amepanda katika kipando, amekaa, au amelala popote alipo, iwe nyumbani, njiani, Msikitini, sokoni, na kadhalika.
- Takbira hii inaitwa Takbeer-e-Mursal na Takbeer-e-Mutlaq.
- Ni Sunnah kusoma Takbira baada ya kila Swalah kuanzia Swalah ya Al-Fajr ya siku ya Arafah hadi swalah ya Al-Asr ya Siku ya mwisho ya Tashreeq, iwe Swalah ya Faradhi au Nafl, Ada (inayotolewa kwa wakati unaofaa) au Qada (inayotolewa kwa wakati uliopita); hata kama ni Swalah ya mazishi. Takbira hii inaitwa Takbira-e-Muqayyad.[2]

---

[1] *Tufa al-Muhtaj, juz. 1, uk. 464*

[2] *I'anat al-Talib'een, juz. 1, uk. 446*



www.dawateislami.net

- Mtu akisahau kusoma Takbira mara tu baada ya Swalah, anapaswa kuisoma mara anapokumbuka.
- Pia ni Sunna kusema Takbira mtu anapoona au kusikia mbuzi, ng'ombe au ngamia katika siku kumi za mwanzo za Dhul-Hijjah.[1]

Ili kupata maelezo ya kina kuhusu ubora wa Eid n.k., soma 'Baraka za Eid-ul-Fitr', sehemu ya 'Baraka za Ramadhani' ambayo ni sura ya kitabu 'Faizan-e-Sunnat.'

Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Utuwezeshe kusherehekea Eid kwa kufuata Sunnah na utujaalie baraka ya kuhiji na Eid halisi ya kuiona Madina na vile vile Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara kwa mara.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mpe mtu mwingine kijitabu hiki baada ya kukisoma

Sambaza vitabu na vijitabu vyenye Lulu za Madani vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah wakati wa harusi, nyakati za huzuni, Urs na maandamano ya Milad, jamaa na hafla zingine na upate thawabu. Jenga mazoea ya kutunza vijitabu dukani kwako ili kuwapa wateja bila malipo. Toa nakala za angalau kijitabu kimoja chenye msukumo wa Sunnah au kijitabu cha Lulu za Madani kwa mtu au watoto wanaowasilisha magazeti na uwaambie wazigawie kwa ujirani

[1] *Al-Munhij Al-Qaweem, uk. 326*

wako mara moja kwa mwezi na hivyo kueneza wito wa kuelekea kwenye haki.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Mwenye kunisomea Durud mara moja, Mwenyezi Mungu Mtukufu humteremshia rehema kumi.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Yeyote aliyesahau kunisomea Durood, amesahau njia ya kwenda Peponi.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Yeyote ambaye alisikia kutajwa kwangu na hakunisomea Durood, bila shaka amekuwa na bahati mbaya.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Mwenye kunisomea Durud mara moja asubuhi na jioni mara moja atapata uombezi wangu Siku ya Kiyama.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Yeyote aliyesikia kutajwa kwangu na hakunisomea Durood, alionyesha kutokuwa mwaminifu (asiye na mapenzi).

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Kwa atakaye nisomea Duruud siku ya Ijumaa, nitamfanyia uombezi Siku ya Kiyama..

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Nisomee Durood kwa wingi. Bila shaka huu ni usafi kwako.

Kauli ya Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Nisomee Durood popote ulipo; Durood yako inanifikia.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب          صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

## Kwa ajili ya kuwa muislamu mcha mungu na mwenye kusimamisha sala

Pitisha usiku wako kwenye jitimai ya kuhuisha Sunna ya Daw at-e-islami inayofanyika kila siku ya Alkhamis Kuamkia ijuma a ndani ya mji wako kwa nia ya kutaka radhi za Allah عزوجل pa moja na nia zingine nzuri. Ili upate kujifunza sunna kuwa na kawaida ya kusafiri siku 3 katika Madani Qafilah pamoja na Wapenzi wa Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ والہ وسلم.

Fanya Fikr-e-Madina kwa kujaza kitabu cha Madani In'amat na ukipeleke kwa Zimmedar (msimamizi) wa eneo lako tarehe mosi ya kila mwezi wa Madani.

**Lengo langu la Madani:** 'Nitajitahidi kujirekebisha mwenyew e na watu wa ulimwengu mzima ان شاء اللہ عزوجل.

Kwa ajili ya kujirekebisha wenyewe tunatakiwa tuzifanyie kazi Madani In'amat na kwa ajili ya kuwarekebisha watu wa ulimw engu mzima tunatakiwa tusafiri katika Madani Qafilah.



Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213
Web: www.maktabatulmadinah.com | E-mail: feedback@maktabatulmadinah.com